KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI

# MIFUMO YETU

**Jarida la Mifumo ya TEHAMA ya TAMISEMI**

TOLEO NA. 3 • NOVEMBA 2017 - JANUARI 2018




# Mfumo Ulioboreshwa wa Kuandaa Mipango na Bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa (PlanRep)

*Picha ya mbele: Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Kassim Majaliwa, akizindua rasmi mifumo ya PlanRep na FFARS mjini Dodoma, tarehe 5 Septemba, 2017. (Picha: Mroki Mroki wa Daily News Mtandao).*

*Jarida hili limeandaliwa kwa ushirikiano kati ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3).*

*" Jarida hili limefanikishwa kwa msaada wa watu wa Marekani kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), chini ya Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3). Ofisi ya Rais -TAMISEMI ndiyo itakayowajibika na matokeo ya kazi hii. Jarida hili ni maoni ya Ofisi ya Rais—TAMISEMI, na si lazima liwakilishe maoni ya USAID au Serikali ya Marekani"*

USAID
KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI

**USAID/TANZANIA UIMARISHAJI WA MIFUMO YA SEKTA ZA UMMA**

UHURU NA UMOJA

# Bodi ya Uhariri

## Mwenyekiti

*Eng. Mussa Iyombe*
*Katibu Mkuu – Ofisi ya Rais, TAMISEMI*

## Wajumbe

*Erick Kitali – TAMISEMI*
*Baltazar Kibola – TAMISEMI*
*Rebecca Kwandu – TAMISEMI*
*Desderi Wengaa – PS3*
*Gemini Mtei – PS3*

## Waandishi

*Atley Kuni – TAMISEMI*
*Beatrice Lyimo – Habari Maelezo*
*Octavian F. Kimario – Habari Maelezo*
*Jacqeline Mrisho – Habari Maelezo*
*Frank Mvungi – Habari Maelezo*
*Frank Shija – Habari Maelezo*
*Gladys Mkuchu – PS3*
*Jacqueline Sombe – PS3*

## Mhariri Mkuu

*Leah Mwainyekule – PS3*

## Wahariri

*Erick Kitali – TAMISEMI*
*Atley Kuni – TAMISEMI*
*Gladys Mkuchu – PS3*

## Msanifu Kurasa

*Leah Mwainyekule – PS3*



## Jarida hili hutolewa na:

*Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-TAMISEMI*
*S.L.P 1923*
*Dodoma-Tanzania*
*Simu: (+255) 26 -2321234*
*Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz*
*Tovuti: www.tamisemi.go.tz*
*Blog: blog.tamisemi.go.tz*

## Ndani ya Jarida Hili:

**Tahariri…………………………………………………………………….…….uk 6**

**Faida za PlanRep Iliyoboreshwa kwa Muhtasari…………………………….uk7**

**PlanRep, FFARS Ziwe Suluhu ya Kutoa Taarifa kwa Wakati……...………uk 8**

**PlanRep Yapokewa kwa Mikono Miwili………..……………………………..uk 9**

**Tanzania ya Kwanza Kusini mwa Afrika Kutumia PlanRep..………………uk 10**

**Maafisa Vituo vya Afya Waomba Mafunzo ya Kompyuta.…………………uk 11**

**PlanRep Yatajwa Kuongeza Ufanisi Katika Sekta za Umma…..…………....uk 12**

**PlanRep Iliyoboreshwa Kutatua Changamoto za Afya Kigoma.………………..uk 13**

**Mfumo wa Kielektroniki Kusaidia Serikali Kuokoa Mabilioni..…………….uk 14**

**PlanRep Yalenga Kurahisisha Kazi ya Kuhudumia Wananchi……………..uk 15**

**PS3 Yataka Usimamizi Imara Mifumo Sekta za Umma……………………...uk 16**

**PlanRep Iliyoboreshwa Kuokoa Sh. Bil. 4 Maandalizi ya Bajeti...…………...uk 17**

**‘Mifumo ya Kielektroniki Kuokoa Muda, Matumizi ya Fedha’……...………uk 18**

**Mfumo wa PlanRep Unathamini Wataalam wa Ndani...……………………..uk 19**

**Wafanyakazi 250 wa Halmashauri Wapatiwa Mafunzo Moro..……………..uk 20**

**PlanRep Iliyoboreshwa ni ya Kipekee………………..…………………......uk 21**

**Madaktari Mtwara Wafurahia Mfumo wa PlanRep………….....…………...uk 22**

**PlanRep Kuongeza Morali ya Watumishi Sekta ya Afya…..…………………uk 23**

**Matukio ya Uzinduzi wa Mifumo katika Picha…….. ………………………..uk 24**

*TAHARIRI:*

# PlanRep Iliyoboreshwa ni Kichocheo cha Maendeleo

Dhana ya kuwashirikisha wananchi katika kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo imepata nguvu kupitia mfumo wa PlanRep iliyoboreshwa. Huu ni mfumo wa kielektroniki unaotumika katika kupanga bajeti, kuandaa mipango na kutoa taarifa ya yale yatakayokuwa yametekelezwa katika eneo husika kwa kuzingatia kuwa msingi wa mfumo huu ni kuongeza kasi katika kuwaletea maendeleo wananchi wenye uhitaji zaidi.

Tunaposhuhudia mageuzi haya makubwa na kuanza kutumika kwa mfumo huu kuanzia mwaka wa fedha 2018/19, ni vema tukatambua kwamba mpango huu unaotekelezwa na Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana na Mradi wa Uimarisha wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), unalenga kuboresha usimamizi wa fedha za Serikali katika ngazi za kutolea huduma kama vile zahanati, vituo vya afya, hosipitali na shule.

Matokeo ya kuboreshwa kwa mfumo huu ni kichocheo cha maendeleo, kwani awali rasilimali nyingi zilitumika katika mchakato wa kuandaa mipango na bajeti. Kwa sasa hali hiyo itakuwa tofauti kwani kila kitu kitafanyika kielektroniki katika mfumo huu wa kitaifa ulioboreshwa kwa maslahi ya wananchi wote hasa waishio maeneo ya vijijini na pembezoni.

Kwa sasa tutashuhudia rasilimali fedha zilizokuwa zikitumika kuandaa bajeti zikielekezwa katika kuboresha huduma za jamii kama shule, zahanati, na ujenzi wa miundombinu itakayosaidia wananchi kuongeza uzalishaji katika maeneo yao, hali itakayochochea kuongezeka kwa pato la mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Mfumo wa PlanRep ulioboreshwa unaendana na matakwa ya sasa ya kisera, kiteknolojia, kiuchumi na umezingatia changamoto zilizokuwepo awali kabla ya kutengenezwa kwa mfumo huu na mahitaji mapya ya wadau na wananchi kwa ujumla wao yamezingatiwa. Hili litawezesha kupatikana kwa matokeo tarajiwa katika kuwahudumia wananchi.

Katika kuandaa mfumo huu, wadau mbalimbali wameshiriki zikiwemo wizara kama OR-TAMISEMI, OR-Utumishi, Wakala ya Serikali Mtandao, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Wizara zingine za Kisekta.

Tunapoangalia faida za mfumo huu ulioboreshwa tunaiona Tanzania mpya, hasa kwa kuwa matarajio ya wananchi ni kuona mageuzi makubwa kama haya ya mifumo yanaleta matokeo chanya katika huduma za jamii katika sekta zote.

Baadhi ya faida za mfumo huu ni pamoja na kuwawezesha watoa huduma kupanga mipango na bajeti kwa kuzingatia mahitaji ya wananchi wa eneo husika, na pia kuwepo kwa uwezo wa kutoa taarifa ya utekelezaji wa mipango na maendeleo.

Mfumo huu pia utaunganishwa na mifumo mingine wakati utakapoanza kutumika, hali itakayosaidia kuongeza tija katika mifumo husika na huduma kwa wananchi. Aidha, mfumo huu utawezesha kutolewa kwa taarifa mbalimbali zinazotakiwa na sekta mbalimbali. Taarifa hizo zitapaswa kuoanishwa na mipango, bajeti na matumizi ili visomwe kwa pamoja.

Kuwepo kwa muundo unaofanana wa uwasilishaji wa bajeti kuanzia ngazi ya msingi, yaani watoa huduma hadi ngazi ya OR-TAMISEMI na Wizara ya Fedha na Mipango, unafanikisha lengo la kuleta matokeo chanya katika kuandaa na hatimaye kutekeleza bajeti katika mwaka husika.


Wakati Tanzania ikichukua hatua kuelekea kuwa nchi ya viwanda na uchumi wa kati, tunaamini kwa dhati kwamba mradi huu wa PS3 ambao unafadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), utaimarisha mifumo na kuleta mabadiliko chanya katika utoaji huduma kwa jamii, hasa zile zenye uhitaji zaidi.


Karibu kusoma jarida hili.


**Eng. Mussa Iyombe**
**Katibu Mkuu, OR-TAMISEMI**

# Faida za PlanRep Iliyoboreshwa kwa Muhtasari

1. Mfumo umetengenezwa kutokana na changamoto zilizopo, mahitaji ya watumiaji na mabadiliko ya kisera, majukumu, teknolojia na muundo.
2. Umetengenezwa na Watanzania wanaojua hali halisi ya uundaji wa mipango, bajeti na uhitaji wa taarifa.
3. Taarifa za bajeti na mipango zinapatikana ngazi zote za utawala kuanzia ngazi ya msingi mpaka ngazi ya Taifa.
4. Mfumo unatoa taarifa kwa mahitaji ya wadau wote ndani na nje ya Serikali.
5. Umefungamanishwa na mifumo mingine ya kimkakati ya Kitaifa kama Mfumo wa Usimamizi wa Matumizi ya Fedha za Umma (IFMIS-Epicor), Mfumo Shirikishi wa Usimamizi wa Watumishi (HCMIS-Lawson), Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato ya ndani ya Halmashauri (LGRCIS) pamoja na Mfumo wa Uhasibu na Utoaji Taarifa kwa Vituo vya Kutolea Huduma (FFARS).
6. Uwezo wa kufanya mapitio ya bajeti na kutoa mrejesho (Auto-Scrutinization).
7. Uwepo wa data moja kwa ngazi zote (Data Integrity and Consistency).
8. Uwezo wa kutunza data za zamani na kufanya ulinganishi (Keeping historical data, Performing comparative and Trend Analysis).
9. Uwepo wa mpango na bajeti za vituo vya kutolea huduma.
10. Utoaji sahihi wa taarifa za utekelezaji (Physical Implementation Report).
11. Mfumo utakuwa na toleo moja nchi nzima. Utaweza kupatikana na wote (Centralized and Unified System).
12. Mfumo unakuwa na sekta zote ndani ya Hlamashauri.
13. Kupunguza gharama za zoezi la uandaaji wa mipango na bajeti kwa asilimia 50.
14. Kupunguza muda wa kufanya zoezi la uandaaji mipango na bajeti kutoka zaidi ya miezi mitatu hadi mwezi mmoja.
15. Umiliki wa mfumo ni asilimia 100 kwa Serikali.
16. Maboresho yanafanyika kwa haraka pasipo gharama.








***Baadhi ya picha zilizochukuliwa kutoka kwenye kompyuta, zikionyesha namna mfumo ulioboreshwa wa PlanRep ulivyo.***

## *KUTOKA DODOMA:*

# PlanRep, FFARS ziwe Suluhu ya Kutoa Taarifa kwa Wakati – Mhe. Majaliwa



***Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), akitoa hotuba ya uzinduzi wa mifumo na PlanRep na FFARS mjini Dodoma. (Picha: Hilary Bujiku wa Ofisi ya Waziri Mkuu).***

Serikali imewataka watumishi wa Mikoa, Halmashauri na vituo vya kutolea huduma kutoa taarifa za mapato na matumizi kwa wakati kwa wananchi katika maeneo yao, ili kuongeza uwazi.

Hayo yamesemwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa Majaliwa, wakati akizindua mfumo uliooreshwa wa kielektroniki wa kuandaa mipango na bajeti kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa (PlanRep), na mfumo mpya wa uhasibu na utoaji taarifa za fedha za vituo vya kutoa huduma (FFARS).

"Ukamilishaji wa mifumo hii utasaidia kuongeza uwazi, uwajibikaji kwa watumshi hasa katika eneo la mapokezi na matumzi ya fedha za umma kuanzia katika vituo vya kutolea huduma mpaka ngazi ya Halmashauri," amesema Waziri Mkuu, katika hafla hiyo ya uzinduzi iliyofanyika mjini Dodoma mwezi Septemba mwaka huu.

"Kuanzia sasa sitarajii kuona kituo chochote cha kutolea huduma kilicho chini ya Halmashauri kinakuwa na matumizi yasiyo zingatia taratibu na kanuni za fedha, au kubadilisha matumizi ya fedha bila kuwasiliana na mamlaka husika," amesisitiza Waziri Mkuu.

Aidha, amesema kwamba lengo la matumizi ya mifumo ya TEHAMA ni kuongeza uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika utendaji kazi wa shughuli za Serikali, na isitumike kukwamisha shughuli na utaratibu wa kazi za Serikali.

Vilevile, Waziri Mkuu amesema kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kipindi kirefu zimekuwa zikitumia gharama kubwa na muda mwingi katika kukamilisha zoezi zima la uandaaji wa mipango, na bajeti, na hivyo kupitia mifumo iliyozinduliwa, changamoto hizo zimetatuliwa.

Kwa upande wake, aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mhe. George Simbachawene, amesema kwamba kupitia mfumo wa PlanRep, zaidi ya shilingi milioni nne zitaokolewa, gharama ambayo Serikali ilizokuwa ikitumia kila mwaka kwa ajili ya kufanya maandalizi ya kuandaa bajeti.

"Mifumo hii itasaidia kuleta ufanisi na uwajibikaji katika utekelezaji wa huduma kwa wananchi. Itasaidia kupunguza muda na kuleta maendeleo kwa kasi, na pia itasaidia kutunza taarifa za mapato yote katika ngazi ya Halmashauri," ameongeza Mh. Simbachawene.

Kaimu Balozi wa Marekani nchini, Bi Imni Patterson, amesema kwamba pamoja na mifumo hiyo kuongeza ufanisi na kuboresha usimamizi wa fedha, itawezesha pia Serikali ya Tanzania kutoa fedha kwa malengo yaliyokusudiwa na mahitaji ya wananchi kwa ufasaha.

"Marekani inajivunia kushirikiana na Tanzania, hasa mnapofanya kazi kwa malengo ya kuwa na Serikali yenye uwazi, maendeleo endelevu na ustawi wa pamoja," amesema Bi Patterson.

***Inaendelea ukurasa wa 9***

*KUTOKA MWANZA:*

# PlanRep Yapokewa kwa Mikono Miwili

Washiriki wa mafunzo ya mfumo ulioboreshwa wa kuandaa mipango na bajeti za Serikali za Mitaa yaliyofanyika Mkoani Mwanza mapema Agosti mwaka huu, wameipongeza na kuishukuru Serikali kwa kuamua kuboresha mfumo wa PlanRep.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, washiriki wa mafunzo hayo wamesema mfumo huo mpya wa kielektroniki utarahisisha utendaji kazi kwa watumishi wa umma katika idara mbalimbali, ikilinganishwa na mfumo uliokuwepo awali. Wamesema mfumo huo utapunguza usumbufu kwa maafisa wa Serikali kusafiri umbali mrefu kwa ajili ya kuwasilisha taarifa na mipango ya bajeti ya Serikali.

“Kwa kutumia mfumo huu tunaweza kuandaa na kutuma taarifa mikoani na wizarani moja kwa moja kutoka katika Halmashauri na vituo vyetu vya kazi,” amesemea Dkt. Hamadi Nyembea, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Msalala, huku akikiri mfumo kuja kwa wakati muafaka.

Amesema kuwa mfumo huu ni rafiki kwa matumizi ukilinganishwa na mfumo uliokuwepo awali, ambao uliwalazimu wakati mwingine kusafiri nje ya kituo cha kazi kwa zaidi ya mwezi mzima kwa ajili ya kuandaa na kuwasilisha taarifa na mipango ya bajeti wizarani.

Amongeza kwamba mfumo huu ni jumuishi, hivyo utawezesha bajeti za idara zote kuwasilishwa kwa wakati mmoja tofauti na ilivyokuwa hapo awali.

“Mfumo huu utaongeza uwajibikaji wa wakuu wa idara na vitengo mbalimbali, hivyo kuongeza tija katika kuwahudumia wananchi,” ameeleza Dkt Nyembea, na kuwapongeza wawezeshaji wa mafunzo na OR-TAMISEMI pamoja PS3 kwa namna walivyowapatia mafunzo mazuri katika hatua mbalimbali, kwa kuwapatia mazoezi ya kutosha yaliyowezesha kuwajengea uzoefu mkubwa. Ameahidi kutumia mafunzo hayo kama sehemu ya kuwawezesha wengine waliopo ofisini.

Mbali na kupongeza, Dkt. Nyembea ameiomba Serikali kuhakikisha kila Halmashauri inapata mtandao wa intaneti ili kuwezesha mfumo huu kufanya kazi kwa ufanisi.

Akizungumza kwa niaba ya washiriki wenzake, Afisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, Bi Sylvia Rwehabura, amewashukuru wawezeshaji kwa kuwapatia mafunzo mazuri kuanzia ngazi ya kupanga, kuanda bajeti na kutoa taarifa.

”Mafunzo haya yametujengea uwezo mkubwa na yametuwezesha kuelewa mfumo huu ulioboreshwa, hivyo kila mmoja wetu ataweza kwenda kuandaa bajeti ya idara yake kwa urahisi,” amesema Bi Rwehabura.

Mafunzo hayo ya siku nane yaliyofanyika mkoani Mwanza yamefadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Marekani (USAID) chini ya Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Sekta za Umma (PS3) na kushirikisha mikoa sita ya kanda ya ziwa ambayo ni Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Mara, Geita na Kagera.

Zaidi ya watumiaji 1,500 tayari wamekwisha patiwa mafunzo hayo hadi Oktoba 2017 kwa kuwahusisha maafisa mipango, wahasibu, wachumi, maafisa tehama na makatibu wa afya wa Halmashauri.

***Na Octavian F. Kimario, Habari Maelezo***



*Baadhi ya washiriki wa mfumo wa PlanRep wakati wa mafunzo. (Picha: Jacqueline Sombe wa PS3)*

***KUTOKA KIGOMA:***

# 'Tanzania ya Kwanza Kusini Mwa Afrika Kutumia Mfumo wa PlanRep'

Tanzania imetajwa kuwa nchi ya kwanza kusini mwa Afrika kwa kuwa na mfumo wa kielektroniki wa kuandaa mipango na bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa (PlanRep) ambao unajumuisha sekta zote katika mfumo mmoja utakaosaidia katika kupanga mipango ya bajeti na kutoa ripoti ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo nchini kote.

Mkuu wa Timu ya Mifumo ya TEHAMA kutoka mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), Bw. Desderi Wengaa, ameyasema hayo mjini Kigoma, wakati wa mafunzo ya PlanRep kwa watumiaji wa mfumo huo. Ameongeza kwamba mfumo huo utasaidia taifa kufikia maendeleo endelevu na kwa wakati, kwani unawashirikisha wananchi wote, na utaunganishwa na mifumo mingine iliyopo sasa.

"Mfumo huu utawezesha utolewaji wa taarifa za miradi ya maendeleo zinazohusu sekta zote zilizoainishwa katika mipango na bajeti kwa wakati katika kipindi chote cha mwaka," amesisitiza Desderi.

Ameeleza kwamba PlanRep iliyoboreshwa inaunganisha sekta zote katika mfumo mmoja ambao ni wa kitaifa, tofauti na ilivyokuwa awali ambapo kila sekta ilikuwa na mfumo wake ambao haukuwa ukiendana na mahitaji ya wakati na haukuwezesha uchambuzi wa kina kufanyika katika kusimamia rasilimali zilizopo, ikiwemo fedha.

Ameongeza kuwa watumiaji wa mfumo wataweza kutumia mfumo huo popote pale watakapokuwa, kwa kuwa ni wa kitaifa, wa kielektroniki, na utaondoa changamoto ya kuwepo kwa matoleo tofauti tofauti, hali itakayosaidia kurahisisha kazi na kuokoa fedha nyingi zilizokuwa zikitumika kwa watoa huduma wa mifumo iliyokuwepo awali katika Halmashauri na mikoa kote nchini.



***Mkuu wa Timu ya Mifumo ya TEHAMA PS3, Desderi Wengaa, akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya PlanRep mjini Kigoma.. (Picha: Frank Mvungi wa Habari Maelezo)***

Kuwepo kwa mradi wa PS3 kumesaidia wataalam wa TEHAMA na watumiaji wengine wa mfumo huo wakiwemo waganga wakuu, wachumi, maafisa mipango, makatibu wa afya na watoa huduma katika ngazi mbalimbali zikiwemo zahanati, vituo vya afya, hospitali na shule, kujengewa uwezo ili kuimarisha utendaji wao katika kuwahudumia wananchi kwa kutumia mfumo mpya wa PlanRep iliyoboreshwa.

Pia, mfumo huu utaunganishwa na mfumo wa malipo (EPICOR), mfumo wa kukusanya mapato (LGRCIS), mfumo wa kukusanya taarifa za sekta ya afya (DHIS2), mfumo wa fedha (FFARS), mfumo wa rasilimali watu wa LAWSON, na mifumo mingine iliyokuwepo awali amabayo inahusika moja kwa moja katika kuandaa mipango na bajeti katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini.

Mfumo huu pia utawezesha uchambuzi wa bajeti kufanyika kwa njia ya mtandao na hivyo kuiwezesha mikoa, wizara, Halmashuri na taasisi za Serikali kuwa na toleo moja la bajeti, ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa mbalibali.

***Na Frank Mvungi, Habari Maelezo***

## PlanRep, FFARS ziwe Suluhu ya Kutoa Taarifa kwa Wakati

***Inatoka ukurasa wa 7***

Akitoa salamu zake, Mkurugenzi wa Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), Dkt. Emmanuel Malangalila, amesema kwamba mifumo hiyo imeundwa na kutengenezwa na vijana wa Kitanzania kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI, Wakala ya Serikali Mtandao, pamoja na Wizara zingine za kisekta, wakishirikiana na wataalam wa Mradi wa PS3, ambao unafadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia shirika lao la maendeleo ya kimataifa (USAID).

"Mifumo hii miwili itaimarisha uwazi, uwajibikaji na ufanisi wa matumizi ya fedha katika Halmshauri na ngazi za vituo vya kutolea huduma, na hivyo utoaji wa huduma kwa wananchi kuwa bora zaidi," amesema Dkt. Malangalila.

Mradi wa uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3) ni mradi wa miaka mitano ulioanza Julai 2015 na utamalizika 2020. Unafanya kazi katika Halmashauri 93 katika mikoa 13 ya Tanzania Bara, ikiwa na lengo la kutoa msaada wa kitaalam kwa Serikali ya Tanzania kwa ajili ya kuimarisha mifumo ya Serikali katika ngazi ya Taifa na Halmashauri, ili kuboresha utoaji wa huduma za jamii.

***Na Beatrice Lyimo, Habari Maelezo***

*KUTOKA MOROGORO:*

# Maafisa Vituo vya Afya Waomba Kupatiwa Mafunzo ya Kompyuta

Maofisa wa Afya wanaohudumia vituo mbalimbali vya afya mkoani Morogoro wameiomba Serikali kuwapatia mafunzo ya kompyuta ili waweze kumudu matumizi ya mifumo mipya ya kielektroniki inayowalazimu kutumia kifaa hicho.

Ombi hilo limetolewa na Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya cha Uhuru mkoani Morogoro, Dkt. Oresta Mwambe, alipokuwa akielezea changamoto wanazozipata kwa kutumia mfumo wa zamani wa kuandaa mipango na bajeti ya Serikali wakati huu wanaposubiri kuanza kutumia mfumo mpya ulioboreshwa ujulikanao kama 'PlanRep' unaohusisha matumizi ya kompyuta.

Dkt. Mwambe amesema kwamba maboresho yanayofanywa na Serikali ni ya msingi kwa kuwa yanaenda kupunguza changamoto nyingi zilizokuwa zinajitokeza wakati wa kuandaa bajeti na mipango ya Serikali, kwani muda mwingine maafisa husika walikuwa wanatumia fedha zao binafsi ili kuhakikisha wanamaliza kazi kwa wakati.

"Mfumo ulioboreshwa wa PlanRep utatusaidia sana kupunguza changamoto zilizokuwa zikijitokeza, lakini changamoto itakayotokea baada ya mfumo mpya kuanza rasmi kutumika ni uhaba wa elimu juu ya matumizi ya kompyuta, kwa sababu maafisa wengi tumezoea kuandaa bajeti kwa njia za kawaida. Tunaiomba Serikali itusaidie japo mafunzo ya awali ili tuweze kutumia mfumo huo kwa ufasaha," ameeleza.

Dkt. Mwambe amefafanua kwamba wakati wa uandaaji wa bajeti utoaji wa huduma kwa wagonjwa unapungua kwa sababu lazima baadhi ya madaktari washiriki katika uandaaji huo, hivyo endapo mafunzo hayo yatatolewa yataenda kuwa mkombozi kwa utoaji bora wa huduma hasa za afya, kwani ni huduma muhimu kwa wananchi.

Naye Mganga Mfawidhi wa kituo cha afya cha Mafiga, Dkt. Sufian Msuya, amesema kwamba maandalizi ya bajeti kwa mfumo unaotumika sasa yanahitaji muda mwingi na gharama kubwa hadi kukamilika kwake, kwa sababu lazima viwekwe vikao mbalimbali na kuchapisha matoleo mengi ili kuhakikisha kazi inafanyika kwa uhakika.

"Tumekuwa tukitumia muda na gharama nyingi kufanikisha bajeti zetu kufika katika Halmashauri, hivyo mfumo wa PlanRep utakuja kuwa mkombozi. Lakini kwa upande mwingine, tunahitaji msaada wa vitendea kazi vitakavyotuwezesha kutumia mfumo huo, ambavyo asilimia kubwa ya vituo vya afya hatuna," amesema Dkt. Msuya.



*Mmoja wa maafisa kutoka kituo cha afya katika wilaya ya Buhigwe mkoani Kigoma, akizungumzia matumizi ya mifumo yatakavyosaidia utendaji kazi katika sekta ya afya. (Picha: John D. Lyimo wa True Vision).*

Ili kuweza kutumia mfumo wa PlanRep vizuri, Mganga Mfawidhi wa kituo cha afya cha Sabasaba, Dkt. Said Mbwana, ameiomba Serikali kuajiri wahasibu na watu wa TEHAMA katika vituo vya afya, kwani kwa sasa kazi za uhasibu katika vituo hivyo zinafanywa na madaktari wenyewe. Kutokana na hilo, inakuwa vigumu kwa madaktari kufanya kazi kwa kutumia baadhi ya mifumo inayohitaji wahusika wa uhasibu na TEHAMA.

"Tunaomba Serikali itusaidie kutuwekea wataalam wa uhasibu na TEHAMA ili madaktari tufanye kazi ya udaktari ambayo ndiyo tuna utaalam nayo. Pia kwa vile tunafanya kazi zote za kuandaa bajeti na mipango ya Serikali basi tuwe tunapewa mafunzo ya upangaji wa bajeti hizo, kwani pia utaalam huo hatuna," amesema Dkt. Mbwana.

Mafunzo ya siku nane ya Mfumo ulioboreshwa wa kuandaa Mipango na Bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa (PlanRep) kikanda yametolewa mkoani Morogoro kwa waandaaji wa bajeti wa Halmashauri mbalimbali za mikoa ya Pwani, Morogoro, Arusha na Kilimanjaro, ambapo yalifunguliwa na Katibu Tawala wa mkoa wa Morogoro.

Mafunzo hayo halihusisha kwa upande wa Mkoa: Mganga Mkuu, Katibu wa Afya, Afisa Mipango, na Afisa TEHAMA. Kwa upande wa Halmahsauri: Mganga Mkuu, Afisa Mipango, Katibu wa Afya, Afisa TEHAMA, na Mhasibu.

***Na Jacqueline Mrisho, Habari Maelezo***

## *KUTOKA MBEYA:*

# PlanRep Yatajwa Kuongeza Ufanisi katika Sekta za Umma




***Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Bi Mariam Mtunguja, akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya PlanRep na FFARS yaliyofanyika jijini Mbeya. (Picha: Frank Shija wa Habari Maelezo).***

Mfumo ulioboreshwa wa uandaaji wa mipango na bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa (PlanRep) umeelezwa kuja wakati muafaka, na kwamba utaongeza ufanisi na uwajibikaji katika utendaji kazi wakati wa kuandaa mipango na bajeti hadi katika utekelezaji wake.

Hayo yamebainishwa na Afisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi mkoani Iringa, Bw. Ambwene Isaya, wakati wa mafunzo ya PlanRep kwa watumiaji wa mfumo huo jijini Mbeya.

Amesema kwamba kutokana na kuwepo kwa utaratibu mzuri wa utendaji kazi kupitia mfumo huo, kila mhusika atawajibika kwa wakati, jambo ambalo litarahisisha utekelezaji wa majukumu na utoaji wa huduma kwa wananchi.

“Sisi tunauona mfumo huu ulioboreshwa kwamba utasaidia sana katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yetu katika kila ngazi ya utekelezaji,” amesema Isaya.

Akizungumzia changamoto watakazokabiliana nazo, ameeleza kwamba kutokana na mfumo huu kufanyakazi kwa uwepo wa mtandao, ikitokea mtandao uko chini kazi zitasimama. Amesema pia kwamba itawalazimu watumiaji kufahamu matumizi ya TEHAMA kwa ufasaha, jambo ambalo wengine linaweza kuwa changamoto kwao kutokana na kutopenda kwenda na wakati.

Akitoa ulinganifu kati ya mfumo wa awali na huu ulioboreshwa, Mchumi Mkuu kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Adam Msumule, amesema kwamba mfumo wa awali ulikuwa hautoi fursa ya mtumiaji kufanya kazi akiwa mbali na kompyuta iliyowekwa programu maalum, jambo ambalo halipo kwa sasa, kwani utakuwa ni kwa njia ya mtandao ambapo mtu ataweza kufanya kazi yake akiwa mahali popote.

Msumule ambaye pia alikuwa mmoja wa watoa mafunzo ya PlanRep iliyoboreshwa, ameongeza kwamba kupitia mfumo huo suala zima la uwazi na uwajibikaji litaongezeka, kwani kila mhusika atapaswa kutekeleza wajibu wake ipasavyo na kwa wakati kwakuwa mfumo umetengenezwa kwa namna ambayo mtu anaweza kujifanyia tathmini ya utendaji wake.

“Kupitia mfumo huu mpya itakuwa rahisi sana kufuatilia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo na matumizi ya fedha zilizoidhinishwa katika miradi husika kwakuwa utakuwa fungamanifu na mifumo mingine kama ule wa Epicor, tofauti na mfumo wa zamani, ” amefafanua Msumule.

Kwa upande wake, Mkuu wa Timu ya Mifumo ya Fedha wa PS3, Dkt. Gemini Mtei, amesema kwamba ili kuhakikisha wanakabiliana na changamoto ya kila idara kutumia mfumo, PS3 imeunganisha mfumo wa mawasiliano ya mtandao ya ndani kupitia mtandao kiambo (LAN), ambapo takribani Halmashuri 69 za Tanzania bara zimeingizwa katika mpango huo.

Katika kuhakikisha watumiaji wa mfumo huu wanajengewa uwezo, Serikali kupitia OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na USAID-Tanzania/PS3 imeendesha mafunzo katika maeneo mabalimbali nchini kuhakikisha inawafikia walengwa ili kujiweka tayari kwa matumizi ya mfumo huo pindi utakapozinduliwa rasmi.

***Na Frank Shija, Habari Maelezo***

***KUTOKA KIGOMA:***

# PlanRep Iliyoboreshwa kutatua changomoto za Afya Kigoma

Mfumo ulioboreshwa wa kuandaa mipango, bajeti na taarifa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa (PlanRep) umekuwa chachu kwa watumishi wa sekta ya afya katika kutoa huduma bora kwa wananchi mkoani humo tangu kuanza kutekelezwa kwa mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3).

Hayo yamesemwa na Katibu wa Afya wa Manispaa ya Kigoma-Ujiji, Bw. Shomari Magijina, katika mahojiano maalumu na mwandishi wa makala hii. Ameongeza kwamba mfumo huu ulioboreshwa utawawezesha watumishi katika sekta ya afya kutoa kipaumbele kwa mahitaji ya zahanati, vituo vya afya na hosipitali, kwa kuhakikisha kuwa yanatimizwa kwa wakati. Vilevile, mfumo utasaidia kuboresha mipango na bajeti za sekta hiyo katika ngazi ya wilaya.

"Kwa mafunzo haya niliyopata kuhusu PlanRep iliyoboreshwa na rasilimali zilizopo katika manispaa yetu, nina uhakika tutaweza kupanga na kutekeleza mipango dhahiri itakayoweza kukidhi matakwa ya kila Halmashauri," amesisitiza Shomari.



***Muuguzi kutoka Kituo cha Afya cha Ujiji Kilichopo Manispaa ya Kigoma-Ujiji akitoa huduma . Kituo hichyo ni moja ya vituo ambavyo vinaendelea kufanya maboresho makubwa ya afya katika Manispaa hiyo . (Picha: Frank Mvungi, Habari Maelezo)***

Naye Bi. Nyangeta Majami, ambaye ni Katibu wa Afya Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, amezungumzia mfumo huo wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo watumiaji yaliyofanyika mjini Kigoma. Nyangeta amesema kuwa ana matumaini makubwa na PlanRep iliyoboreshwa kwani itaanza kuleta mageuzi makubwa katika sekta hiyo, hasa utoaji wa huduma bora kwa wananchi.



***Bi. Nyangeta Majami, Katibu wa Afya Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, Kigoma, akiwa mwenye furaha wakati wa Mafunzo ya PlanRep Mkoani Kigoma. (Picha: Frank Mvungi, Habari Maelezo)***

"Nimeipokea PlanRep iliyoboreshwa vizuri kwa sababu itaongeza tija kwa kiasi kikubwa, hasa kwenye suala la muda uliokuwa ukitumika kuandaa mipango na bajeti, Vilevile, PlanRep itaunganishwa na mifumo mingine kama DHIS 2 ambayo tunaitumia katika ukusanyaji wa taarifa katika sekta ya afya," amesema.

Kutokana na mahitaji mapya ya wadau na changamoto zilikuwepo awali katika mfumo uliopita wa PlanRep, Mradi wa PS3 kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI pamoja na OR-Utumishi, Wizara ya Fedha, Wizara ya Afya, Mikoa na Halmashauri, wameweza kuungana na kufanya maboresho makubwa katika mfumo huo ili uweze kuendana na mahitaji ya sasa ya kisera, kiteknolojia na kiuchumi.

Dhumuni la kushirikisha wizara, mikoa na Halmashauri katika kutekelzeza mradi huu ni kuhakikisha kuwa Tanzania inapata mfumo imara wa mipango na bajeti utakaoweza kukidhi mahitaji ya wakati, kwani mfumo huu unawezesha Halmashauri kutekeleza majukumu yake, Zaidi ya mipango na bajeti, utawezesha pia kuainisha vyanzo vya mapato kwa Halmashauri, kufuatilia fedha zilizoingia, utekelezaji wa mipango pamoja na matumizi yake.

***Na Jacqueline Sombe, PS3***

## *KUTOKA MTWARA:*

# Mfumo wa Kielektroniki Kusaidia Serikali Kuokoa Mabilioni

Serikali inatarajia kuokoa mabilioni ya shilingi kutokana na kuanza kwa matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa kuandaa mipango na bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa (PlanRep), ambapo kabla ya kuboreshwa kwa mfumo huu wastani wa kiwango cha fedha kilichotumika kilikuwa takribani milioni hamsini kwa kila Halmashauri kila mwaka.

Akizungumza wakati wa mafunzo maalum kuhusu mfumo huo yaliyofanyika mjini Mtwara, Afisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea Mkoani Ruvuma, Bw. Shaban Millao, amesema fedha zitakazopungua ni zile zilizokuwa zikitumika kulipa watumishi wa Halmashauri na mikoa masurufu ya safari, gharama za mafuta ya magari, uchapishaji wa nyaraka mbalimbali wakati wa mchakato wa kuandaa bajeti pamoja na uwasilishaji wake, ambapo kwa sasa kazi hii itafanyika katika mfumo wa kielektroniki.



*Afisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Bw. Shaban Millao, akizungumza wakati wa mahojiano maalum kuhusu mfumo wa PlanRep na faida zake. (Picha: Jacqueline Sombe wa PS3).*

"Gharama za kuchapisha tu vitabu vya bajeti na mipango katika Halmashuri zetu kwa wastani ni milioni 4 kwa kila mwaka, hivyo unaweza ukaona kiasi cha fedha kitakachookolewa kwa kuwa mfumo wa sasa utakuwa wa kielektroniki ambao sasa unaondoa sehemu ya gharama zilizokuwa zinatumika awali katika mchakato huu," amefafanua.

Shaban amesema kwamba mfumo huo unawawezesha maafisa mipango kutekeleza majukumu yao popote pale, na utasaidia kuimarisha mawasiliano katika ngazi zote za Serikali kwa kuwa upatikanaji wa taarifa mbalimbali kuhusu mipango ya idara na Halmashauri kwa ujumla utakuwa rahisi na wenye kuendana na mahitaji ya wakati.

Ameongeza kuwa mfumo huu uliooreshwa umejikita katika kusaidia kupanga, kuandaa bajeti na kutoa taarifa ya utekelezaji, hali itakayosaidia kuongeza tija na usimamizi wa rasilimali zinazoelekezwa katika huduma za jamii kutokana na bajeti iliyopangwa katika mwaka husika.

"Wito wangu kwa Serikali ni kuwa mikoa na Halmashauri zote ziunganishwe katika mfumo huu ambao utaleta mapinduzi makubwa katika sekta zote za huduma za jamii, ikiwemo elimu na afya," ameongeza Shaban.

Ameipongeza pia OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na mradi wa PS3 unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), kwa kufanikisha kuwepo kwa mfumo wa kitaifa utakaochochea maendeleo, hasa kwa wananchi wenye uhitaji zaidi.

Watumishi watano waliopatiwa mafunzo ya mfumo huo wa kieektroniki wataweza kutoa mafunzo kwa watumishi wengine wa Halmashauri, hivyo mpango wa Halmashauri utaoanisha na kuhusianisha sekta zote. Kutokana na zoezi la uandaaji wa mipango kuwa shirikishi, itawapa fursa wananchi kushiriki mipango husika.

"Mfumo huu unalazimisha kila mtumishi kutimiza wajibu wake katika eneo lake na hakutakuwa na visingizio tena katika kuandaa mipango, bajeti, kutekeleza na kutoa ripoti kwa wakati," amesisitiza Amon, na kuongeza: "Ni wakati muafaka kwa watumishi wote katika Halmashauri kuwa na mtazamo wa pamoja katika mageuzi haya yanayolenga kuwainua wananchi wenye uhitaji zaidi kwa kuwapatia huduma bora."

***Na Jacqueline Sombe, PS3***

*KUTOKA MWANZA:*

# PlanRep Yalenga Kurahisisha Kazi ya Kuhudumia Wananchi



*Mmoja wa washiriki wa PlanRep kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, Amosy Zephania, akiongea wakati wa mahojiano maalum juu ya matumizi ya mfumo wa PlanRep. (Picha: John D. Lyimo wa True Vision).*

Mfumo ulioboreshwa wa kuandaa mipango na bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa (PlanRep) unalenga kurahisisha kazi ya kuwahudumia na kuwapelekea maendeleo wananchi.

Hayo yamesemwa na Dkt. Leonard Subi, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, wakati akifunga mafunzo ya siku nane ya jinsi ya kutumia mfumo wa PlanRep. Mafunzo hayo yalifanyika jijini Mwanza, na yalihusisha mikoa sita ambayo ni Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Geita, Mara na Kagera.

Akizungumza na washiriki wa mafunzo hayo, Dkt. Subi ameeleza kwamba lengo kuu la mfumo huo ni kuleta ufanisi katika kuwahudumia walengwa wakuu walioko chini ya mamlaka za Serikali, ambao ni wananchi. Amesema mfumo huu unawaleta pamoja watumishi kuhakikisha kuwa mipango yote ya Halmashauri inawalenga wananchi.

Sambamba na hilo, Dkt. Subi ameishukuru Serikali kwa mpango wa kuweza kutoa fedha moja kwa moja kwa vituo vya kutolea huduma kwa wananchi.

”Kwa wale tulioanza mpango wa malipo kwa ufanisi, tumeshuhudia mabadiliko makubwa sana kwa shilingi milioni 10 tulizozipeleka katika vituo vyetu vya kutolea huduma. Kwa muda mfupi sana tumeona mabadiliko na wananchi wameanza kushuhudia matunda na kazi kubwa ya Serikali na wao kushiriki kama wamiliki wa vituo hivi,” ameeleza Dkt. Subi.

Ameongeza kwamba matumizi ya mfumo huu yanapunguza kwa kiasi kikubwa gharama za kusafiri umbali mrefu kwa ajili ya kupeleka taarifa, badala yake taarifa sasa zinaweza kupelekwa mikoani na wizarani kwa njia ya mtandao.

”Mwaka huu tumekaa Dodoma karibu mwezi mmoja na nusu tunaandaa mipango ya afya. Tumekuwa tukitumia gharama kubwa sana. Kwa kutumia mfumo huu wa mtandao sasa, itarahisisha mawasiliano na mtu atakaa kwenye kituo chake akiandaa mpango na kuutuma kwa njia ya kielektroniki,” amesema.

Aidha, amewaasa wale wote waliopatiwa mafunzo hayo kuendelea kuutumia mfumo wa PlanRep ili kujengea uwezo wengine, na kutanabahisha kwamba mfumo huu ni wa Serikali na unasimamiwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, na kwamba mafunzo yameshirikisha wadau wote muhimu katika suala zima la bajeti.

Dkt. Subi amewashukuru Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) kwa kufadhili mafunzo hayoa kupitia Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3).

Akitoa salaam za wizara kabla ya kufunga mafunzo hayo, Ndugu Elisa Rwamiago, Afisa Msimamizi wa Fedha Mwandamizi kutoka Ofisi ya Rais – TAMISEMI, ameelezea kwamba mafunzo hayo yatatolewa kwa mikoa na Halmashauri zote nchini.

Mfumo huu mpya wa PlanRep umezingatia changamoto zilizojitokeza katika mfumo uliokuwa ukitumika awali. Mfumo wa awali ulianza kutumika takribani miaka kumi iliyopita, lakina umekuwa na changamoto mbalimbali, jambo lililoelekea kushindwa kuandaa na kusambazwa kwa wakati kwa taarifa na mipango ya bajeti za Serikali za Mitaa hapa nchini.

***Na Octavian F. Kimario, Habari Maelezo***

## *KUTOKA MBEYA:*

# PS3 Yataka Usimamizi Imara Mifumo Sekta za Umma

Katika kuhakikisha nguvu inaongezeka katika usimamizi wa mifumo yote ya sekta za umma, mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), umejipanga kuwajengea uwezo watumiaji wa mifumo hiyo katika eneo la usimamizi ili ifanye kazi kwa ufanisi na kuwa endelevu hata mara baada ya mradi huo kumaliza muda wake ifikapo 2020.

Hayo yamebainishwa na Mkuu wa Kitengo cha Mifumo ya Fedha wa Mradi wa PS3, Dkt. Gemini Mtei, katika mahojiano maalum wakati wa mafunzo kwa ajili ya watumiaji wa mfumo mpya wa uandaaji wa mipango na bajeti katika Serikali za Mitaa (PlanRep), jijini Mbeya hivi karibuni.

Dkt. Mtei amesema kwamba mpaka sasa wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa kufanya maboresho katika mifumo mbalimbali iliyokuwa inatumiwa na Serikali, na kuongeza kuwa jambo kubwa la kutilia mkazo kwa sasa ni namna ambavyo mifumo hiyo itasimamiwa ili iwe endelevu.

"Jambo ambalo sasa tunatarajia kulitilia mkazo zaidi ni eneo la usimamizi wa mifumo ya sekta za umma. Tunataka kuona mifumo hii ikiendelea hata baada ya mradi wetu wa PS3 kumaliza muda wake," amesema.

Kutambua umuhimu wa usimamizi wa mifumo, PS3 iliona haja ya kuendelea na mifumo ile iliyokuwepo badala ya kuja na mifumo mipya, jambo ambalo limewezesha Serikali kuendelea kuwa msimamizi wa karibu wa mifumo hiyo. Mafunzo hayo ya PlanRep ni matokeo ya changamoto zilizoainishwa na watumiaji (wafanyakazi wa Serikali) ambao walibainisha maeneo ambayo wangependa yafanyiwe maboresho.

Dkt. Mtei amezitaja changamoto hizo kuwa ni pamoja na matumizi makubwa ya rasilimali fedha itokanayo na mchakato mzima wa uandaaji wa bajeti kuanzia ngazi ya kijiji, ambapo inahusisha rasilimali watu ambao wote wanahitaji kugharamiwa.

Amesema pia kwamba baada ya kuainishwa kwa changamoto hizo, TAMISEMI walikuja na mapendekezo ya kuufanyia maboresho mfumo huo ambao umekuja kutatua changamoto hizo. Utatuzi mmojawapo ni kupunguza gharama kwa kurahisisha mawasiliano kwa njia ya kielektroniki badala ya mtu kufunga safari kutoka sehemu moja hadi nyingine. Vilevile, kupitia mfumo huo mtumiaji ataweza kufanya marekebisho ya bajeti yake au taarifa yake bila ya kuchapisha nakala yote, jambo linalopunguza gharama.

Kwa upande wake, Mtaalamu wa Masuala ya TEHAMA kutoka OR-TAMISEMI, James Mtatifikolo, amesema kuwa Serikali kupitia ofisi hiyo ndiyo yenye dhamana ya kuisimamia mifumo hiyo baada ya kujengewa uwezo kwa kupitia msaada wa PS3.

Mtatifikolo ameeleza kuwa maboresho hayo ya mifumo, hasa wa PlanRep, ni kwa mujibu wa mahitaji ya Sera ya TEHAMA na miongozo mbalimbali ya Serikali.

Pamoja na kuwa mradi wa huu PS3 unatekelezwa katika Mikoa 13 na Halmashauri 93 za Tanzania Bara, bado manufaa yake yanazifikia Halmashauri zote kupitia miradi mbalimbali inayotekelezwa.

Katika muendelezo wa kuwajengea uwezo watumiaji wa mifumo iliyofanyiwa maboresho ya Serikali kwa kushirikiana na USAID/Tanzania chini ya mradi wa PS3, mafunzo yameendeshwa nchi nzima, na yameshirikisha watumiaji wa mifumo ya PlanRep na mfumo wa utoaji taarifa za fedha (FFARS).

***Na Frank Shija, Habari Maelezo***




***Mkuu wa Timu ya Mifumo ya Fedha PS3, Dkt. Gemini, akitoa mada wakati wa mafunzo ya mifumo ya PlanRep na FFARS yaliyofanyika jijini Mbeya. (Picha: Frank Shija wa Habari maelezo).***

***KUTOKA DODOMA:***

# PlanRep Iliyoboreshwa Kuokoa Sh. Bil.4 Maandalizi ya Bajeti




***Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa (Mb) (kushoto) na Kaimu Balozi wa Marekani hapa nchini, Bi. Inmi Patterson, wakifuatilia matukio mbalimbali wakati wa uzinduzi wa mifumo mjini Dodoma (Picha: Mroki Mroki wa Daily News Mtandao).***

Septemba 5, 2017 Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), aliandika historia mpya katika ulimwengu wa Serikali za Mitaa Tanzania kwa kuzindua mifumo miwili: mfumo wa kuandaa mipango, bajeti na taarifa kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa (PlanRep), na mfumo wa uhasibu na utoaji taarifa za fedha katika vituo vya kutolea huduma (FFARS)

Akizungumza katika uzinduzi huo, aliyekuwa Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI, Mhe. George Simbachawene (Mb), amesema katika mchakato wa mipango ya bajeti kwa Halmashauri 185 ya Tanzania bara, takribani sh. bilioni 8.32 zilikuwa zikitumika kila mwaka kwa ajili ya maandalizi ya bajeti.

Amesema fedha hizo hutumika kulipia usafiri (mafuta), posho ya kujikimu, shajala na gharama za kurudufu vitabu. "Gharama hizo hazijumuishi gharama za mawasiliano ya mtandao, umeme, simu, matengenezo ya magari na matengenezo ya vifaa," ameongeza Mhe. Simbachawene.

Amebainisha kuwa kutokana na gharama hizo, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimepata wakati mgumu kwa kujikuta zikitumia fedha nyingi kugharamia maandalizi ya bajeti na kusababisha wananchi kukosa huduma kutokana na wataalam wa Halmashauri kutumia muda mrefu katika mchakato huo,

"Mbali ya gharama hizi, wataalam wetu walitumia muda mwingi nje ya maeneo yao ya kazi. Maandalizi ya bajeti yamekuwa na changamoto nyingi na kusababisha Halmashauri kuvuka na bajeti kubwa mwisho wa mwaka, kwa kuwa zoezi huchukua muda mrefu. Lakini sasa hii PlanRep itaweza kuokoa Sh.Bil.4," amefafanua.

Mifumo hiyo iliyozinduliwa na Waziri Mkuu, inalenga kuimarisha uwazi, uwajibikaji na ufanisi wa matumizi ya fedha katika Halmashauri na katika ngazi ya vituo vya kutolea huduma, na hivyo utoaji huduma kwa wananchi kuwa bora zaidi.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), amesema ukamilishwaji wa mifumo hiyo utasaidia kuongeza uwazi na uwajibikaji kwa watumishi, hasa eneo la mapokezi na matumizi ya fedha za umma. "Hii ni kuanzia katika vituo vya kutolea huduma za elimu na afya mpaka katika ngazi ya Halmashauri," amesema.

"Kwa kuzingatia sera ya ugatuaji wa madaraka kwa wananchi (D by D) na kupitia utaratibu wa Serikali Kuu kupeleka fedha za matumizi ya kawaida na shughuli za maendeleo moja kwa moja katika vituo vya kutolea huduma za afya, mifumo hiyo itasaidia kusimamia mapato na matumizi sahihi ya fedha za Serikali na kuleta maendeleo ya haraka kwa wananchi," ameongeza.

Waziri Mkuu ameeleza kwamba mifumo hiyo ambayo imesanifiwa na kuboreshwa inamilikiwa na kusimamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia OR-TAMISEMI kwa asilimia 100, na kwamba mfumo wa PlanRep ni rafiki, fungamanifu, na hautakuwa na matoleo mapya ya mara kwa mara na una manufaa makubwa ya kuwezesha Halmashauri zote nchini kutoa taarifa zenye *'format'* sahihi na kwa urahisi zaidi.

"Mifumo hii miwili itaunganisha idara na vitengo ndani ya Halmashauri na kuwezesha wataalam wanaoandaa taarifa za uandaaji wa Mipango na Bajeti pamoja na utekelezaji wake wafanye kazi kama timu moja kwa kuwa mifumo hii imejumuisha matakwa na mahitaji ya sekta zote zilizoko katika Halmashauri zetu," ameongeza.

Waziri Mkuu amesema kwamba kuanzia sasa hatarajii kuona kituo chochote cha kutoa huduma za elimu na afya kilichopo chini ya Halmashauri kinakuwa na matumizi yasiyozingatia taratibu na kanuni za fedha za umma au kubadilisha matumizi ya fedha bila kuwasiliana na mamlaka husika.

Ameeleza kuwa matumizi ya fedha yafanyike kutegemea chanzo cha fedha kilichopokelewa kwa wakati na kwa mujibu wa bajeti iliyotengwa kwa mwaka husika. "Nitapenda OR-TAMISEMI na ofisi yangu zipate taarifa zote za mipango, bajeti pamoja na taarifa za fedha zinazopelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa wakati, na zikiwa katika ubora wa hali ya juu," amesema Mhe. Majaliwa.

Aidha, Mhe. Waziri Mkuu ameagiza matumizi ya mifumo hii kwa wadau wote, na iwapo kuna hitaji jipya mifmo hii iboreshwe, na sio kuanzisha mifumo mingine. Vilevile, taarifa za mipango, bajeti na matumizi kutoka katika mifumo hii ziingizwe katika tovuti za Halmashauri na Mikoa kupitia mfumo wa tovuti wa Serikali (GWF) uliozinduliwa Machi 2017, kwa ajili ya Halmashauri na Mikoa yote nchini.

Ameagiza kuwa mapungufu na dosari zinazojitokeza wakati wa ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka za Halmashauri zitatuliwe kupitia mifumo hiyo.

***Na Atley Kuni, OR-TAMISEMI***

## *KUTOKA MWANZA:*

# 'Mifumo ya Kielektroniki Kuokoa Muda, Matumizi ya Fedha'

Uandaaji wa mipango na bajeti umepitia mifumo tofauti na misimu mbalimbali, ambapo awali watumiaji walikuwa wakitumia mashine ya kuchapa '*Facit*' na hivyo kutumia mda mrefu sana katika uandaaji, na mara zote kuwepo kwa marekebisho mengi yaliyolazimisha kurudiwa kwa uchapaji wa taarifa za Halmashauri.

Akiyasimulia hayo, Afisa Mipango kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi, Jommo Paul Watae, amesema: "Tulipokuwa na PlanRep ya awali ilikuwa ina changamoto tofauti, sababu ilibidi kukusanyika kwenda Dar es Salaam kwa kipindi kirefu katika kuaandaa mipango. Ilikuwa lazima kuwa na rasilimali fedha za kujikimu na vilevile za kuwezesha kuchapa kopi na kudurufu taarifa hizi."

Watae ameeleza kwamba mfumo ulioboreshwa wa kuandaa bajeti, mipango na taarifa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa, utawezesha kuokoa matumizi makubwa yaliyokuwa yanatumika, na fedha hizo kuweza kutumika katika matumizi yaliyokusudiwa ya kuhudumia wananchi.

"Itaokoa pia muda, kwasababu PlanRep ya kielektroniki imerahisisha mchakato mzima wa uandaaji wa mipango na bajeti na kila kitu kuweza kukamilika kwa muda mfupi ikiwemo uandaaji, marekebisho na mrejesho, hivyo tutatumia muda mfupi katika kuandaa mipango na bajeti hizi. Hii itasaidia kupata muda wa kutosha wa kuweza kuwahudumia wananchi kwa wakati," ameeleza.

Naye mkufunzi wa kitaifa wa mafunzo hayo ya PlanRep iliyoboreshwa, Bi. Joyce Kalumule kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ameeleza kwamba mafunzo hayo yamelenga kuwafikia watumiaji kutoka katika idara zote zilizopo katika Halmashauri, ambao wataweza kupeleka maarifa hayo kwa watumiaji wengine wa mfumo katika Halmashauri.

"PlanRep iliyoboreshwa itapunguza muda, ambao hapo awali iliwabidi watumishi wa Halmashauri kutoka kwenye vituo vyao vya kazi na kwenda kukaa mahali kwa siku nyingi kwa ajili ya kuandaa hii mipango. Lakini kuanzia sasa kila kitu kitafanyika katika mtandao wakiwa maeneo yao ya kazi," amesema.



***Mmoja wa wawezeshaji, Bi. Joyce Kalumule kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, wakati wa mahojiano maalum juu ya matumizi ya mfumo wa PlanRep. (Picha: John D. Lyimo wa True Vision)***

Naye Mchumi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, Amosy Zephania, amesema mfumo wa awali wa kuandaa PlanRep ulikuwa unatumia gharama kubwa sana katika uandaaji wake kutokana na hatua mbalimbali zilizokuwa zinapitiwa katika kukamilisha na kuwasilisha mipango.

"Mfumo wa sasa ulioboreshwa wa PlanRep ambao ni wa kielektroniki utawezesha kuokoa rasilimali nyingi zilizokuwa zinatumika hapo awali ambapo ilibidi kutumia muda mrefu sana katika uandaaji wa bajeti na mipango. Ilibidi kutumia gharama katika kuchapisha mipango hii kama shajara na kurudufu, na unaweza kuta kuna masahihisho ukishawasilisha mipango hii ambayo ilitulazimu kusahihisha na kurudia mchakato wa awali na hivyo gharama kuzidi zaidi," ameeleza.

Amosy ameongeza: "Kimsingi rasilimali zinazoletwa na Serikali Kuu kuja Halmashauri au zinazokusanywa na Halmashauri zinalenga katika kumhudumia mwananchi. Sasa iwapo fedha hizi zinakuwa zimetumika katika kuandaa mipango na bajeti, zinaahirisha baadhi ya huduma katika maeneo yetu kama vile za afya, elimu na zingine."

Amekiri kwamba hakuna jambo zuri sana katika Serikali kama kuwa na uthabiti wa mifumo iliyohuishwa na inayozungumza, ili kumfanya mtumiaji kuweza kupata taarifa mbalimbali ambazo anahitaji. Hii ni kwasababu zinapatikana katika mtandao, na itasaidia Halmashauri kuweza kupanga na kuandaa bajeti zenye uhalisia zaidi kulingana na taarifa zilizopo na kuwezesha mwananchi kupatiwa huduma kulingana na mahitaji.

***Na Gladys Mkuchu, PS3***

## *KUTOKA MWANZA:*

# Mfumo wa PlanRep Unathamini Wataalam wa Ndani

Mfumo ulioboreshwa wa kuandaa Mipango na Bajeti za Mamlaka ya Serikali za Mitaa (PlanRep) umeanza kuundwa tangu mwezi Februari, 2017 na wataalam wa ndani ya nchi, kutoka mfumo wa zamani ambao umetumika kwa zaidi ya miaka 10 sasa.

Mshauri wa Mifumo ya TEHAMA wa PS3, Bi. Nseya Kipilyango, ameyasema hayo katika mahojiano maalum wakati wa mafunzo ya mfumo ulioboreshwa wa PlanRep mkoani Mwanza.

"PlanRep imetengenezwa na timu ya wataalam wa ndani, yaani Watanzania, na hatujaajiri mtu yeyote kutoka nje ya nchi. Kazi hii tumeifanya kwa pamoja kwa kushirikiana na TAMISEMI, Wakala ya Serikali mtandao, pamoja na wizara nyingine za kisekta," amesema.

Nseya ameelezea hatua mbalimbali zilizofuatwa katika uundaji wa mfumo, ambazo ni kushirikisha wadau katika kupata mahitaji ya mfumo. Zoezi hilo lilifanyika mjini Morogoro na kuweza kushirikisha wadau toka ngazi za msingi kama vile watendaji wa kijiji, kata pamoja na watoa huduma katika sekta ya afya na elimu.

Washiriki wengine wa awali walitoka katika kada mbalimbali za Halmashauri na pia ofisi za mikoa, OR-TAMISEMI, Wizara ya Afya, Wizara ya Maji, Wizara ya Kilimo, na Wizara ya Fedha. Kutokana na ushiriki huo, washiriki wote ambao ndio watumiaji wakubwa wa mfumo waliweza kushirikishwa kuanzia mwanzo, na wao ndio waliotoa mahitaji ambayo yametokana na changamoto wakati wanatumia mfumo wa awali wa PlanRep.

> ***"Hapo awali Maafisa TEHAMA tulikuwa tukionekana kama mafundi tu wa kompyuta na vifaa vingine vya kielektroniki"*** **- Isaack Tanguye, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela**

Kwa upande wake, Isaack Tanguye ambaye ni Afisa TEHAMA wa Manispaa ya Ilemela, amesema kwamba mbali na kutumia wataalam wa hapa hapa Tanzania katika uandaaji wa mfumo wa PLANREP, utekelezaji wa mfumo huu katika ngazi za Halmashauri pia umeweza kuthamini majukumu ya wataalam mbalimbali kama vile maafisa TEHAMA ambao wamepewa majukumu makubwa katika kuhakikisha kuwa mfumo unafanya kazi vizuri.

"Hapo awali Maafisa TEHAMA tulikuwa tukionekana kama mafundi tu wa kompyuta na vifaa vingine vya kielektroniki, lakini tunashukuru mfumo huu wa PLANREP iliyoboreshwa umewezesha kuonekana kwa mchango wetu katika utekelezaji wa majukumu, na hasa katika matumizi ya teknolojia za mitandao na mifumo mingine ya kielektroniki," ameeleza.

***Na Gladys Mkuchu, PS3***




***Baadhi ya wataalam wa Tanzania ambao walihusika katika uundaji wa PlanRep iliyoboreshwa, wakiwa katika picha ya pamoja wakati wa uzinduzi wa mfumo huo mjini Dodoma. (Picha: Mroki Mroki wa Daily News Mtandao).***

*KUTOKA MOROGORO:*

# Wafanyakazi 252 wa Halmashauri Wapatiwa Mafunzo ya PlanRep Morogoro

Jumla ya wafanyakazi 252 wa Halmashauri mbalimbali kutoka Mikoa ya Pwani, Morogoro, Kilimanjaro na Arusha, wamepata mafunzo ya Mfumo ulioboreshwa wa kuandaa Mipango na Bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa ujulikanao kama PlanRep, yaliyofanyika mkoani Morogoro.

Haya yameelezwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Miundombinu ya TEHAMA kutoka OR-TAMISEMI, Eng. Baltazar Kibola, wakati wa mafunzo hayo.

Kibola amesema kwamba mfumo huo sio mpya, lakini umeboreshwa kwa kuongezewa vitu muhimu vitakavyoshughulikia mapungufu yaliyokuwa yakitokea katika mfumo wa zamani, hali iliyosababisha kudhoofika kwa utoaji wa huduma kwa wananchi.

"Mfumo huu ulikuwa ni mfumo unaojitegemea; haukuweza kusambaza taarifa katika ngazi mbalimbali za Serikali wala kushirikisha watoa huduma kutoka mapendekezo yao yatakayoongeza uboreshaji wa mipango na Bajeti za Serikali, hivyo kwa kuwa tumeuboresha ni wazi kwamba watumiaji wa mfumo huu wanatakiwa kupewa mafunzo," ameeleza Kibola.



***Mmoja wa washiriki wa mafunzo ya mfumo wa PlanRep akifuatilia kwa makini wakati mada zikiendelea kutolewa kwenye mafunzo hayo. (Picha: Mroki Mroki wa Daily News Mtandao).***

Ameongeza kwamba katika mradi huo, OR-TAMISEMI imejikita katika kuratibu utengenezaji wa mfumo huo, kuandaa mafunzo katika mikoa mbalimbali ambayo imepangwa kwa ajili ya kufanyia mafunzo, na kutafuta wataalam wa TEHAMA pamoja na wawezeshaji na kuhakikisha vifaa vya TEHAMA vinakuwepo.



***Mwezeshaji wa mafunzo ya mfumo wa PlanRep, Christopher Masaaka, akitoa maelekezo kwa wakufunzi wakati wa mafunzo ya mfumo huo. (Picha: Morki Mroki wa Daily News Mtandao).***

Naye mmoja wa wawezeshaji wa mafunzo hayo, Christopher Masaaka, amesema kwamba asilimia kubwa ya watumiaji wa mfumo wameyapokea vizuri mafunzo hayo kwani mfumo huo unakwenda kurahisisha uandaaji wa mipango na bajeti zinazoandaliwa kila mwaka ambazo zilikuwa zikitumia muda mwingi na gharama kubwa katika maandalizi yake.

"Washiriki wamefanya vizuri katika mafunzo; wameweza kupanga mipango kutoka ngazi ya vituo, idara, Halmashauri, Mikoa hadi wizara kwa majaribio, pia wameweza kuandaa na kufanya uchambuzi wa mipango na bajeti kupitia mfumo huo," amesema Masaaka.

"Hivi sasa itakuwa rahisi sana kupata *'historical data'* pamoja na kufanya ulinganifu wa taarifa na utekelezaji wa bajeti katika ngazi mbalimbali.

Aidha, ametoa rai kwa Serikali kuongeza nguvu na jitihada zaidi kwa kuweka miundombinu ya TEHAMA na kutoa mafunzo kwa ajili ya kuwajengea uwezo watumiaji katika ngazi zote, ili matumizi ya mfumo huo yaweze kuleta matunda mazuri.

***Na Jacqueline Mrisho, Habari Maelezo***

***KUTOKA DODOMA:***

# PlanRep Iliyoboreshwa ni ya Kipekee - Rumanyika



***Mmoja wa wawezeshaji wa mfumo wa PlanRep, Digna Zenda, akitoa mafunzo kwa washiriki mjini Dodoma (Picha: Mroki Mroki wa Daily News Mtandao).***



***Afisa TEHAMA wa Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe, Edward Rumanyika, akizungumza wakati wa mahojiano maalum juu ya matumizi wa mfumo wa PlanRep. (Picha: Jacqueline Sombe wa PS3)***

Mfumo wa kielektroniki wa PlanRep iliyoboreshwa umetajwa kuwa shirikishi na ambao unawapa nafasi watu wa ngazi zote za utendaji Serikalini kushiriki katika kuandaa bajeti, kuanzia kwenye ngazi ya vituo vya kutolea huduma hadi ngazi ya Halmashauri, kisha ngazi ya mkoa na hata taifa.

Kauli hiyo imetolewa na Afisa TEHAMA wa Halmashuri ya Wilaya ya Ukerewe Mkoani Mwanza, Bw. Edward Rumanyika, wakati wa mahojiano maalum kuhusu mafunzo ya matumizi ya mfumo wa kuandaa mipango, taarifa na bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa (PlanRep) yaliyofanyika mkoani Dodoma.

"Hatua hii itasaidia kupunguza muda wa kuandaa bajeti, ambapo awali tulikuwa tunatumia takribani miezi mitatu kwa ajili ya shughuli hiyo. Vilevile, PlanRep ya awali haikuwa shirikishi na iliishia ngazi ya wakuu wa idara pekee," ameeleza.

Rumanyika amesema kwamba mfumo wa sasa ulioboreshwa unazungumza na mtumiaji, tofauti na ilivyokuwa hapo awali ambapo mfumo haukuwa rafiki kwa watumiaji. "Ukiangalia katika *'navigation'* kwa mfano, mtumiaji akiingia kwenye mfumo unamuongoza katika kila hatua na kumuwezesha kila mtumiaji kuona vipengele kutokana na matumizi yake katika mfumo," amefafanua.

> ***"Kwa mfumo huu tutatendea haki maendeleo ya teknolojia ambayo ni kwa ajili ya kusaidia kuongeza tija na kuleta matokeo chanya."*** **- Edward Rumanyika, Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe**

Mfumo una uwezo wa kutoa mrejesho, kwani mtumiaji mmoja akiwa kwenye mfumo na akikamilisha majukumu yake mtumiaji mwingine anaweza kuona kazi iliyofanyika, na endapo kutakuwa na changamoto inaweza kutatuliwa kwa wakati huo huo. Pia, mfumo unawapa uwezo watumiaji kuwasiliana ndani ya mfumo hivyo kuepuka gharama za kuchapisha mipango na bajeti ambazo hazijakamilika kama ilivyokuwa hapo awali.

Akizungumzia faida za mfumo huo, Rumanyika amesema kwamba utachochea uwazi, uwajibikaji na tija kwa watendaji katika mikoa, Halmashauri na vituo vya kutolea huduma. Kwa kupunguza gharama za kuandaa mipango, bajeti, na ripoti, rasilimali nyingi zitaelekezwa katika kutoa huduma kwa wananchi na utekelezaji wa mipango mbalimbali ya maendeleo.

"Kwa mfumo huu tutatendea haki maendeleo ya teknolojia ambayo ni kwa ajili ya kusaidia kuongeza tija na kuleta matokeo chanya kama haya ya PlanRep iliyoboreshwa," ameeleza Rumanyika, na kuongeza: "Watu wote wakitimiza wajibu wao kama mfumo unavyotaka, basi tutaweza kuandaa na kufanikisha maandalizi ya bajeti ya kila Halmashauri ndani ya kipindi cha mwezi mmoja tu.

Mafunzo ya PlanRep iliyoboreshwa yamefanyika kwa siku nane kwa watumishi wa Umma ambao ni maafisa TEHAMA, wachumi, maafisa mipango, makatibu wa afya wa miko ana Halmashauri, waganga wakuu wa mikoa na Halmashuri, na wahasibu. Mafunzo yamekuwa yenye manufaa kwa watumiaji hao kutokana na maboresho yaliyofanyika ambayo yataleta mageuzi makubwa katika kuandaa bajeti, mipango na kutoa taarifa za mikoa na Halmashauri zote nchini.

***Na Jacqueline Sombe, PS3***

## *KUTOKA MTWARA:*

# Madaktari Mtwara Waufurahia Mfumo wa PlanRep

Madaktari wameipongeza Serikali na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Marekani (USAID), kwa kutekeleza mradi wa Uimarishaji wa Mifumo Katika Sekta ya Umma (PS3) wenye lengo la kuleta mageuzi katika kupanga mipango ya Halmashauri na bajeti zake kwa kutumia mfumo wa kielektroniki.

Akizungumza katika mahojiano maalum wakati wa hafla ya ufunguzi wa mafunzo ya kuwajengea uwezo watumiaji wa mfumo wa kuandaa mipango, bajeti na utoaji taarifa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa (PlanRep) Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Dkt. Charles Mkombe, amesema mfumo huo ni mageuzi makubwa katika sekta ya afya kwakuwa utasaidia kuongeza tija katika kuwahudumia wananchi na utakuwa shirikishi.

''Mfumo huu utaunganisha watoa huduma wote kuanzia ngazi ya kata zikiwemo shule, zahanati, vituo vya afya, Halmashauri na OR-TAMISEMI, hivyo nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwasababu sasa utekelezaji wa bajeti na mipango utaenda kama ilivyopangwa, hali itakayoongeza uwajibikaji kwa wananchi tunaowahudumia katika maeneo yetu,"

Dkt. Mkombe ameeleza kuwa faida za mfumo huo ni kuwaongezea ujuzi madaktari katika kuandaa bajeti, na utakuwa chachu ya kufanya maboresho katika kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma, yakiwemo majengo ya kutunzia dawa. Hali hiyo itachochea na kukuza huduma zinazotolewa kwa wananchi katika sekta zote, ikiwemo afya.

"Faida nyingine za mfumo huu ni kuokoa muda, rasilimali fedha na kuwapa muda wa ziada watoa huduma katika kuwahudumia wananchi, maana hawatalazimika kusafiri ili kuratibu maandalizi ya bajeti na mipango ya Halmashauri zao," ameongeza.

Aidha, Dkt. Mkombe amesema kuwa mfumo wa awali haukuwa rafiki kwa watumiaji kwasababu muundo wa mfumo huo ulitofautiana kutoka Halmashauri moja hadi nyingine, ambapo zaidi ya miezi minne ilitumika kuandaa bajeti na haukuwa wazi kwa wananchi katika kupanga na kuamua vipaumbele vyao. Pia, kulikuwa na upotevu mwingi wa fedha.



***Baadhi ya washiriki wa mafunzo ya mifumo ya PlanRep na FFARS wakifuatilia kwa vitendo mfumo huo wakati wa mafunzo yaliyofanyika mjini Mtwara. (Picha: Jacqueline Sombe wa PS3)***

Naye Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Madaba mkoani Ruvuma, Dkt. Mustafa Waziri, amesema kuwa mafunzo kuhusu PlanRep iliyoboreshwa yamewajengea uwezo wa kusimamia bajeti katika maeneo yao, wakianza na kuimarisha usimamizi wa rasilimali fedha maana maandalizi na utekelezaji wa bajeti unaanzia ngazi ya kituo cha kutolea huduma.

Ameongeza kwamba tangu kuanza kwa mradi kumekuwa na mageuzi na mafanikio katika utendaji wa mikoa na Halmashauri kutokana na uimarishwaji wa mifumo unaofanyika ukilenga kuongeza tija.

Mafunzo ya mfumo wa PlanRep yalienda sambamba na ya mfumo wa utoaji taarifa za fedha katika ngazi ya kituo, ambao kwa lugha ya Kiingereza unajulikana kama *'Facility Financial Accounting Reporting System'* (FFARS). Mafunzo ya mfumo wa FFARS yatawasaidia watoa huduma katika ngazi ya vituo kusimamia rasilimali fedha, hali itakayosaidia kutekelezwa kwa sheria na taratibu za manunuzi na utoaji taarifa.

***Na Frank Mvungi, Habari Maelezo.***

***KUTOKA MTWARA:***

# PlanRep Kuongeza Morali ya Watumishi Sekta ya Afya

Mfumo uliooboreshwa wa kuandaa Mipango na Bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa (PlanRep), umetajwa kuwa kichocheo cha kuongeza morali kwa watumishi wa sekta ya afya nchini kutokana na kuongeza uwazi na ushirikishwaji wa wananchi katika kusimamia rasilimali fedha.



***Muuguzi katika kituo cha Afya cha Likombe kilichopo Mtwara-Mikindani akimsaidia mama aliyejifungua katika kItuo hicho. Kituo hicho kinachokua kwa kasi katika mji wa Mtwara kutokana na maboresho yanayoendelea kufanywa na Serikali katika sekta ya afya na wadau mbalimbali wa maendeleo. (Picha: Jacqueline Sombe wa PS3)***

Wakizungumza katika mahojiano maalum mjini Mtwara, baadhi ya watumishi wa sekta ya afya wamesema wanafarijika kuona kuwa sasa Serikali imeongeza bajeti ya huduma za Afya ikiwemo dawa, na kuanza uimarishaji wa miundombinu katika vituo vya kutolea huduma kama zahanati, vituo vya afya na hospitali zote nchini.

Akifafanua, muuguzi wa kituo cha afya Likombe cha mjini Mtwara, Bi. Mwisa Mkumbo, amesema kuwa kwa sasa Serikali imerudisha morali ya watumishi wa sekta hiyo kwa kuboresha mazingira ya kazi, hali inayosaidia wananchi kupata huduma bora za afya katika kituo hicho kinachokua kwa kuzingatia maboresho ya miundombinu yakiwemo majengo, vifaa tiba, watumishi, na utaratibu mpya wa mfumo wa kielektroniki utakaoanza kutumika.

"Kutokana na kukosekana kwa uwazi hapo awali katika kupanga mipango na bajeti, huduma katika maeneo mengi hazikufikia viwango vinavyotakiwa, hali iliyosababisha Serikali kupoteza rasilimali nyingi na hivyo kukosekana kwa thamani halisi ya fedha katika miradi iliyotekelezwa," amesema Bi. Mkumbo

Ameongeza kuwa hata wananchi wa chini kwa sasa watanufaika na mfumo huo utakapoanza kutumika, kwakuwa utawezesha upatikanaji wa fedha kwa wakati na kamati za afya zitashiriki kikamilifu kusimamia matumizi ikiwa ni sehemu ya matokeo ya mradi wa PlanRep iliyoboreshwa.

Kwa upande wake, Mganga Mkuu wa kituo hicho, Dkt. Victor Andrea, amebainisha kuwa mfumo wa zamani haukuwa unazingatia vipaumbele vya watoa huduma na hawakuwa na uwezo wa kufanya mageuzi, ambapo mfumo mpya umekuja na kuwa suluhisho la changamoto zilizokuwepo awali katika mfumo uliokuwa ukitumika.

"Tunaamini mfumo huu utaondoa kwa kiasi kikubwa malalamiko ya wananchi kuhusu huduma za afya ambapo katika kituo chetu tumejipanga vizuri kuhakikisha tunatoa huduma bora kupitia mfumo huu mpya utakaokuwa chachu ya kuleta mabadiliko kwa watumishi wote wa sekta ya afya na jamii inayotuzunguka," amesema Dkt. Andrea.

Aidha, amesema kituo cha afya Likombe ni kituo kinachokua kwa kasi katika mji wa Mtwara kutokana na maboresho yanayoendelea kufanywa na Serikali katika sekta ya afya, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo ambao wameonyesha dhamira ya dhati katika kuboresha huduma zinazotolewa katika vituo vya afya, kikiwemo cha Likombe.

"Kuwepo kwa takwimu sahihi katika vituo vyetu vya afya zinazohusu mahitaji na mipango ni moja ya vichocheo vinavyoweza kuchangia matokeo chanya katika mipango na utekelezaji wake, hasa kwa kutumia mfumo huu wa kielektroniki katika kupanga na kuandaa bajeti," amesisitiza Dkt. Andrea.

***Na Jacqueline Sombe, PS3***

## MATUKIO MBALIMBALI KATIKA PICHA WAKATI WA UZINDUZI WA MIFUMO YA PLANREP NA FFARS MJINI DODOMA






*Kushoto: Waziri Mkuu Mh. Kassim Majaliwa akiteta jambo na Kaimu Balozi wa Marekani nchini, Bi. Inmi Patterson. Kulia: Mkurugenzi wa Mradi wa PS3, Dkt. Emmanuel Malangalia, akitoa salaam wakati wa uzinduzi.*





*Kushoto: Mkurugenzi wa USAID/Tanzania, Andrew Karas pamoja na mawaziri Mh. Ummy Mwalim, Dkt. Philip Mpango, na Mh. Jenista Mhagama, wakifuatilia uzinduzi wa mifumo. Kulia: Msanii Mrisho Mpoto akitoa burudani wakati wa uzinduzi wa mifumo.*





*Kushoto: Elisa Rwamiago wa OR-TAMISEMI akipokea cheti cha pongezi kutoka kwa Waziri Mkuu, Mh. Kassim Majaliwa, kwa kuwa mmoja wa waundaji wa mifumo ya PlanRep na FFARS. Kulia: Baadhi ya wageni waalikwa wakifuatilia hafla ya uzinduzi wa mifumo.*

# MIFUMO YETU